## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2013 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2010, 2011 na 2012.

***Jedwali 7: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2010 hadi 2013***

| | 2010 | | 2011 | | 2012 | | 2013 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 26.38 | 20.12 | 20.77 | 21.89 | 23.37 | 21.99 | 22.89 | 20.98 |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 27 | 20 | 20 | 20 | 24 | 20 | 23 | 20 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 49 | 39 | 47 | 40 | 48 | 39 | 47 | 40 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

a) Alama ya wastani ilishuka kidogo kutoka **23.37** mwaka wa 2012 hadi **22.89** mwaka wa 2013.

b) Alama ya juu iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2013 ni **47** tofauti na **48** ya mwaka wa 2012.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **23** tofauti na **24** ya 2012.

**Katika Insha:**

a) Alama ya wastani ilishuka kidogo kutoka **21. 99** ya mwaka wa 2012 hadi **20.98** mwaka wa 2013.

b) Alama ya juu zaidi iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2013 ni **40** tofauti na **39** ya mwaka wa 2012.


c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20** kama ilivyokuwa mwaka 2012.

d) Alama wastani inaelekea kufikia kiwango kinachokubaliwa **(20/40)** japo imepita kiwango hiki kiasi.



Powered by: www.atikaschool.com


Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.




## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### 4.1.1 Uchanganuzi wa maswali maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali:




### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa

Katika mwaka wa 2013, yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini (30%). Maswali yafuatayo ndiyo yanayochukuliwa kuwa yaliwatatiza wanafunzi zaidi: Swali 3, 7, 11, 16, 32, 36, 38, 39 na 41



Powered by: www.atikaschool.com

*Jedwali 8: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa*

| Maswali | 3 | 7 | 11 | 16 | 32 | 36 | 38 | 39 | 41 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi** | 22.24 | 18.01 | 20.35 | 18.64 | 17.72 | 6.64 | 18.66 | 18.67 | 10.69 |
| **Asilimia ya wastani ya mswali yale mengine** | 23.71 | 26.60 | 24.48 | 24.04 | 25.91 | 20.04 | 25.09 | 23.99 | 22.54 |

### 4.1.3.1 Ruwaza za majibu

**Maswali 1 mpaka 15**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** hadi **15**. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Ufanisi wa mwanafunzi katika masomo humtegemea yeye. Licha ya kuwa mwalimu __1__ katika masuala mengi, uamuzi wa kuzingatia __2__ ya mwalimu huwa wake.

Mwalimu hupitisha maarifa kama vile jinsi ya kutumia lugha kuwasiliana. Mathalani, mwalimu hufunza maneno kama vile halaiki, funda na kikosi ambayo ni __3__. Hali kadhalika, mwanafunzi hufunzwa maadili kama vile ustahimilivu ambao humfanya __4__. Ni dhahiri kwamba mwalimu ana uwezo mkubwa wa __5__ mwanafunzi. Kwa hivyo hana budi kuwa kielelezo kifaacho kwani __6__. Mwanafunzi naye asiwe mlegevu, __7__.

**Swali la 3**

A. nomino za wingi B. nomino za jamii C. nomino za dhahania D. nomino za jumla

**Matokeo ya swali la 3**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 11.04 | 22.24 | 23.13 | 42.47 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.60 | 23.71 | 20.73 | 24.03 |

Swali hili lilitahini nomino za jamii au nomino za makundi. Hata hivyo, watahiniwa wengi, kwa kuona neno **jumla** ,walifasiri **jumla** kuwa **makundi**. Nomino za jumla ni nomino za kawaida wala si nomino za wingi. Ni muhimu walimu kufunza upya aina za nomino ili wanafunzi waache kukanganyika.

**Swali la 7**

A. awe na nia ya kujiimarisha masomoni
B. awe na hakika ya kujiimarisha masomoni
C. awe na ari ya kujiimarisha masomoni
D. awe na matumaini ya kujiimarisha masomoni

**Matokeo ya swali la 7**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 50.41 | 5.26 | 18.01 | 25.18 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23.06 | 17.78 | 26.60 | 21.08 |



Powered by: www.atikaschool.com

Swali hili lilitathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuqanisha maneno katika msururu wa kauli na kuchanganua maana yake.Watahiniwa wengi walichagua jibu **A : awe na nia ya kujiimarisha masomoni** bila kuzingatia neno lililotangulia hili.Mtu anaweza kuwa na nia lakini akawa mlegevu au mvivu.

Ukosefu wa mvua __8__ madhara yasiyomithilika. Ukame unapojiri wanyama na mimea __9__ zaidi na joto. La muhimu kujiuliza ni je, ikiwa wanyama wanaathirika hivyo, __10__ binadamu? Mojawapo ya __11__ hali hii ni hulka ya binadamu ya kutozingatia suala la kuongeza __12__ katika mazingira kwa __13__. Matokeo ya hulka hii ni kwamba watu wengi wameshindwa __14__ hata kwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Wengine wanakuwa maskini ombaomba kwa kuuza ardhi yao __15__.

**Swali la 11**

A. kiini cha     B. hatima ya     C. hatima za     D. viini vya

**Matokeo ya swali la 11**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 44.86 | 24.07 | 9.69 | 20.35 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23,25 | 21.57 | 21.42 | 24.48 |

Swali hili lilitahini wingi.Watahiniwa wengi bado hawajatambua kuwa unapotumia neno **mojawapo,** ina maana kuwa mtu anachagua kati ya vitu anuwai. Kwa hivyo, neno linalofuata sharti liwe katika wingi. Tunasema **mojawapo ya viini** wala si **mojawapo ya kiini**.

**Swali la 16**

*Chagua kielezi katika sentensi ifuatayo*:

Mwanafunzi hodari na mtiifu aghalabu huwapendeza watu wengi.
A.hodari     B.aghalabu     C . mtiifu  D . wengi

**Matokeo ya swali la 16**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 36.19 | 18.64 | 28.04 | 16.03 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.79 | 24.04 | 22.42 | 25.01 |

Swali hili lilitahini matumizi ya vielezi.Yaelekea kuwa wanafunzi wengi hawatofautishi kati ya vivumishi na vielezi.Watahiniwa wengi waliteua neno ***hodari*** ambalo ni kivumishi.



Powered by: www.atikaschool.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31 – 40**.*

Maridhia alikuwa pale jukwaani akiwa miongoni mwa waalikwa mahususi katika shule ya upili ya wasichana ya Twapambazuka. Hii ilikuwa shule ya kipekee iliyokuwa imejengwa hivi majuzi kutokana na michango ya wafadhili na marafiki fulani wa chanda na pete wa Maridhia.

Maridhia alipokuwa pale jukwaani aliwatupia macho wanafunzi waliokuwa wamejaa pomoni pale ukumbini. Kisha akajisemea kimoyomoyo, "Wanafunzi hawa wana bahati ya mtende. Wangejua kilichowapata wasichana wa enzi zetu, katu wasingezembea masomo. Wangejua hatua kubwa iliyopigwa na dada zao wangewaiga na kuzidi kufungua macho na kuikumbatia hamu ya kusoma zaidi. Sijui nitatumia lugha au mbinu gani leo kuwahamasisha!"

Rafikiye Maridhia, aliyekuwa mmoja wa wageni, alipomwona Maridhia kadidimia mawazoni alimgutusha. "Hee! Maridhia, mbona hivyo? Unawazia nini?" Maridhia aliyaficha machozi yaliyokuwa yanayaziba macho yake, machozi yaliyotokana na kumbukumbu ya yale aliyoyapitia hadi kufikia pale. Kisha akajutia purukushani na kumjibu, "Hakuna jambo la maana la kuwazia sasa. Ya kale hayanuki. Sasa nataka nigange yajayo." Wakaendelea kusikiliza hotuba hizi na zile za kusifu hatua mbalimbali zilizopigwa katika kuinua kiwango cha elimu cha wanawake pale pao Shimoni. Mara kwa mara Maridhia alisikia jina lake likitajwa na kumiminiwa sifa kemkem na shukrani tele.

Maridhia alizirudisha fikira zake nyuma tena, akakumbuka vile alivyosoma kwa shida licha ya kuwa wazazi wake hawakuwa wachochole. Alikumbuka vile wazazi hao walivyomnyima fursa ya kujiunga na shule ya upili kwa kufuata misimamo hasi ya wakazi wa Shimoni wa wakati huo. Hawa waliandama fikira kuwa kumsomesha msichana ni kupoteza mali bure. Wazazi wa Maridhia, kwa kuongozwa na tamaa, wakamuoza kwa babu mmoja mkwasi kupindukia. Ilibidi Maridhia akubali uamuzi huu shingo upande. Maridhia alikumbuka jinsi alivyoteseka katika ndoa hiyo. Alikumbuka vipigo vya kila mara, vicheko, vitisho na kuaibishwa hadharani na jamii, hasa ilipotokea kuwa amechelewa **kuipata mbeleko**. Mambo yalipomfika kooni akasema, "Potelea mbali, liwe liwalo, hata wakisema mwacha mila ni mtumwa ni sawa. Maneno matupu hayavunji mifupa." Baada ya kuwaza na kuwazua Maridhia alitafuta maarifa ya kujinasua, akamwendea Bi Salama na kumlilia shida. Bi Salama alimshauri ajiunge na kituo cha elimu ya watu wazima. Huko Maridhia alipewa mafunzo mengi. Alitia shime masomoni akiamini kuwa kisomo hakina umri wala mwisho, akasoma hadi chuo kikuu.

Baada ya kuhitimu chuoni alirudi kwao na kupata kazi ambayo ilimwezesha kuwakimu wazazi wake waliokuwa wazee. Aidha alianzisha miradi mbalimbali Shimoni. Mafanikio ya Maridhia yaliwasuta na kuwaaibisha kindanindani wale waliomdhulumu awali. Wengine walimsingizia hili na lile. Hata hivyo, hawangeweza kufanya lolote kuizima kiu ya Maridhia ya kujiendeleza. Maridhia aliwapuuza akisema kuwa asilani jua haliwezi kuzuiwa kwa ungo.

Miaka mitatu baada ya Maridhia kupata kazi walirudiana na mumewe. Mumewe alimwomba msamaha naye Maridhia akamsamehe. Aliwasamehe pia wote waliomtesa. Aliwaona kuwa walioongozwa na itikadi zilizopitwa na wakati. Aliwaelimisha wanakijiji kuwa ni muhimu kumsomesha mwanamke pia. Wasibague. Mwanamke mmoja akielimishwa, huelimisha dunia. Maneno ya Maridhia yalimtoa nyoka pangoni, watu wakawasomesha wana wa jinsia zote, Shimoni ikaanza kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo. Shule zilijengwa, miundomsingi kama vile barabara ikaimarishwa na hospitali zilizokuwepo zikaboreshwa. Maji ya mabomba yalisambazwa vijijini, chombo kilichokuwa kinaelekea kuzama kikaokolewa.

**Sifa za Maridhia zilivuma pembe zote za Shimoni na jamii jirani.** Wazazi na walezi waliwapigia watoto wao mfano wa Maridhia ambaye aliweza kuzikosoa mila duni na akafaulu. Jambo hilo lilionekana kuwa mwiko hapo awali. Jamii nzima ilifunguka macho; Maridhia akawa kielelezo, si kwa vijana wa kike tu, bali pia kwa vijana wa kiume, wazazi na jamii kwa jumla.



Powered by: www.atikaschool.com

**Swali la 32**

Machozi ya Maridhia yalitokana **hasa** na :

A. kumbukumbu ya mateso aliyokuwa anapitia
B. kumbukumbu ya talaka na ndoa yenye taabu
C. kumbukumbu ya mateso waliyopitia na wenzake
D. kumbukumbu ya mateso na mafanikio yake.

**Matokeo ya swali la 32**

| **Majibu** | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 55.69 | 6.19 | 19.32 | 17.72 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.44 | 20.37 | 22.36 | 25.91 |

Hili ni swali la kiutekelezaji. Mtahiniwa alihitajika kutumia ujuzi wa yaliyomo katika taarifa kuteua jibu sahihi.Watahiniwa wengi waliteua jibu **A,** pengine kwa kuwa kifungu kinataja mateso. Hata hivyo, taarifa inaonyesha hali mbili za maisha ya Maridhia, naye Maridhia anakumbuka yote aliyopitia, mema na mabaya.. Linalojitokeza hapa ni kwamba wanafunzi wengi hawadiriki kusoma vifungu kwa makini.

**Swali la 36**

Kijiji cha Shimoni kilikuwa nyuma kimaendeleo kwa sababu ya:

A. kufuata sana tamaduni na mila zao;
B. kupuuza mchango wa vijana katika maendeleo;
C. kutowazia wito wa vijana kuhusu maendeleo;
D. kuwatia wasichana katika ndoa za mateso.

**Matokeo ya swali la 36**

| **Majibu** | A | **B*** | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 59.64 | 6.64 | 9.69 | 22.89 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 24.78 | 20.04 | 20.51 | 19.93 |

Swali hili lilitahini stadi ya utekelezaji. Mtahiniwa alihitajika kutumia ufahamu wake wa yaliyomo katika kifungu kujibu swali. Hata hivyo, asilimia kubwa ya watahiniwa ilichagua jibu **A.** pengine kwa kuathiriwa na kuwapo kwa neno utamaduni katika kifungu. Hata hivyo, kifungu kinakashifu kufuata mila zilizopitwa na wakati.Watahiniwa hawakuzingatia kwamba Shimoni ilikuwa nyuma kwa kuwabagua wasichana.

**Swali la 38**

**'Sifa za Maridhia zilivuma pembe zote za Shimoni na jamii jirani.'**Methali inayoweza kujumuisha maneno haya ni:

A. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
B. Mkulima ni mmoja walaji ni wengi.
C. Mkuu hukua kwao.
D. Mcheza kwao hutuzwa



Powered by: www.atikaschool.com

**Matokeo ya swali la 38**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 20.63 | 49.25 | 10.32 | 18.66 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.34 | 22.53 | 24.00 | 25.09 |

Swali hili lilipima uwezo wa kusanisi mawazo na kupata maana yake kupitia methali.Watahiniwa wengi walichagua **B** bila kutambua kuwa maana inayojitokeza ni kwamba **Maridhia alisifiwa kwingi,** wala si **matendo ya Maridhia yaliwanufaisha wengi.**

**Swali la 39**

Maana ya **kuipata mbeleko** ni:
A. kujipatia mahitaji ya mtoto;
B. kuwa na matumaini ya ujauzito;
C. kujifungua mtoto;
D. kuwa mjamzito.

**Matokeo ya swali la39**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 14.28 | 18.53 | 18.67 | 47.37 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 19.92 | 20.37 | 23.99 | 24.39 |

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kutumia neno **mbeleko** kupata maana ya nahau. Mbeleko kwa kawaida hubebea mtoto aliyezaliwa, wala haihusishwi na ujauzito kama watahiniwa wengi walivyodhania.Ni muhimu walimu kuwaelekeza wanafunzi kuwazia swali kwanza kabla ya kuteua jibu.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Amani ni hali inayofaa kuenziwa na kuimarishwa kila wakati na kila mahali. Baadhi ya watu huamini kuwa amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga lakini si kweli wakati wote. Amani ya kudumu huweza pia kupatikana kwa njia ya maafikiano.

Ukosefu wa amani una gharama kubwa isiyolipika kwa urahisi. Wahenga waliosema, **"Kama hujui kufa tazama kaburi,"** hawakukosea. Tukitaka kuyajua maafa yaletwayo na vita katika ukanda huu, tuna mifano kemkem. Si nchini, si kwa majirani, twaweza kujifunza mengi kuhusu umuhimu wa amani na hasara zinazoletwa na kinyume chake.

Jamii zinazokumbwa na mizozo hujionea makubwa. Baadhi ya watu waliowahi kuwa mamlakani huweza kupoteza nyadhifa zao; viongozi wa awali wakawa si chochote si lolote. Hali ya utulivu, furaha na maendeleo hutoweka kama moshi. Mambo mengi hutumbukia nyongo. Uharibifu wa mali **hushamiri** na wengi hupoteza milki zao.

Vurugu zinapotokea watu hutoroka, kila mmoja akikimbiza roho yake. Wakati kama huu, mali kama vile **mashamba, majumba ya kifahari, magari mengi, pesa na hata mifugo huwa mizigo mizito isiyobebeka**. Katika hali hii familia hujikuta zimesambaratika. Upweke nao huzidi. Pa kukimbiliwa pia huwa shida. Hali ya utegemezi huibuka. Wakimbizi hutegemea usalama kutokana na ukarimu na ukaribu uliopo kati yao na wahisani wao. Mambo hayawi sawa hata kidogo. Ghafla uhuru anaokuwa nao mtu hutoweka kwani **cha mwenzio hakiwezi kuwa kama chako na huwezi kukitolea sauti**, ni nguo ya kuazima ati.



Powered by: www.atikaschool.com

Watu wakiwa uhamishoni ndipo wanapokumbuka umuhimu wa amani. Wao hujuta na kukumbuka mambo yasiyo na msingi yaliyozua ghasia. Wengi hukumbuka vurumai zilizotokana na tofauti kubwa za kisiasa, kiuchumi na kikabila, ufisadi na tamaa. Wengine huwaza kwa uchungu kuhusu hali ya mali zao walizochuma kwa miaka mingi kuangamizwa kwa sekunde chache tu! Wengi wao hutatizika kimawazo wasijue pa kuanzia wala pa kuelekezea juhudi zao.

Ikumbukwe kuwa ukimbizi nchini au nje ya nchi ni karaha tupu. Mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, maji, makao, mavazi na malazi hukosekana. Magonjwa hatari hukurupuka kila mara. Isitoshe vifo huzidi, sio tu kupitia magonjwa, bali pia kutokana na mapigano na dhiki za kisaikolojia . Wakati huu, uvunjaji wa sheria huzidi na uchumi wa nchi huzorota kwani hata watalii huchelea kuingia nchini kwa sababu ya ukosefu wa usalama. Fahari ya nchi hudidimizwa na kuzikwa kwenye lindi la kina kirefu.

Ili kuhakikisha kuwa jamii zote zinaishi kwa amani, haifai kupakata mikono na kuamini kuwa wazazi, walimu na viongozi ndio ambao hawana budi kujaribu kwa hali na mali kuhubiria umuhimu wa amani na kusameheana. Inatujuzu kujaribu kuibua na kukuza hisia za uzalendo miongoni mwa wanajamii. Elimu nayo ifunze na kusisitiza umuhimu wa kuwa raia wema. Raia wote waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuandama sera na mienendo inayohimiza usawa katika makundi yote ya kijamii. Walio katika mamlaka wawasisitizie vijana umuhimu wa kuungana na raia wengine licha ya tofauti zao za kikabila, kihali na hata kirangi.

**Swali la 41**

Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa kifungu.

A. Amani huweza kupatikana hata palipo na ugomvi.
B. Amani huimarishwa zaidi baada ya maafikiano.
C. Kuwepo kwa amani huwawezesha watu kujifunza mengi.
D. Kwenye amani gharama ya vita hupungua.

**Matokeo ya swali la 41**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 10.69 | 42.85 | 25.80 | 19.54 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.54 | 22.92 | 22.47 | 23.69 |

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kutathmini na kutoa uamuzi ufaao.Hata hivyo, watahiniwa wengi, pengine kwa kutokuwa makini, walikosa kuona kulikokuwa na kiini cha jibu.Wengi walikimbilia jibu **B** ambalo halihusiani na hali ilivyo katika kifungu.

### 4.1.3.2 Hitimisho

Kwa jumla uchanganuzi wa mtihani wa mwaka 2013 umebainisha kwamba utendaji wa wanafunzi katika maswali ya ufahamu unaendelea kuimarika. Asilimia kubwa haikutatizika na maswali ya ufahamu kama ambavyo ilikuwa kawaida katika mitihani ya miaka ya awali. Hata hivyo, bado pana haja ya wanafunzi kufunzwa mikakati bora ya kukabiliana na maswali ya ufahamu.

Kadhalika imebainika kwamba watahiniwa bado wanafanya vyema zaidi katika ufahamu wa kibunilizi ikilinganishwa na utendaji katika ufahamu wa kimaelezo.Ni muhimu walimu kuwaongoza wanafunzi zaidi katika kujibu maswali ya aina zote mbili za ufahamu .Pia wanafunzi wanastahili kuhimizwa kusoma kwa mapana ili kukuza stadi za kukabiliana na maswali ya ufahamu wa kuandika.



Powered by: www.atikaschool.com

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

Katika mwaka wa **2013** mada ya insha ilikuwa:-

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.

Swali hili lilitahini uandishi wa hotuba. Mtahiniwa alihitajika kubuni utungo ambao unaonyesha umuhimu wa usafi.

a) **Maudhui/yaliyomo**

Hapa mtahiniwa alihitajika kuandika hotuba inayoonyesha, ama umuhimu wa usafi wa mwili na mazingira, au madhara yanayotokana na kutodumisha usafi wa mwili na mazingira. Hoja zifuatazo zinaweza kuzingatiwa:

i) kuzuia wadudu waharibifu
ii) kuepuka magonjwa
iii) kufanya mandhari kuvutia
iv) kujiletea sifa
v) kuepuka kutokimbiwa na marafiki
vi) kudumisha utulivu, n.k

b) **Muundo na mtindo**

Muundo wa hotuba ulihitajika kuzingatiwa. Yafuatayo yalitarajiwa kubainika:

i) **Mwanzo** – Hatibu aanze kwa kuwatambua watu kulingana na vyeo.Aliye na madaraka ya juu atajwe mwanzo.Aishukluru hadhira kwa kuhudhuria.Kiini cha hotuba pia kibainishwe hapa.
ii) **Mwili** –Hapa ndipo mtahiniwa anapozikuza hoja kuhusu usafi wa mwili na mazingira.
iii) Mtindo wa hotuba ujitokeze.Hatibu azungumze moja kwa moja na hadhira akiichochea kukubaliana na msimamo wake.Uteuzi mwafaka wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za kimtindo zinazolenga kukuza mada husika uzingatiwe.
iv) Kaida za kisarufi zizingatiwe.
v) Maendelezo mwafaka ya maneno yazingatiwe.
vi) Hotuba iandikwe kwa hati nadhifu inayosomeka.
vii) **Hitimisho-** Hapo ndipo hatibu anapokamilishia hotuba yake. Msimamo wa hatibu ujitokeze. Awashukuru kwa kumsikiliza.

### 4.2.1 Vigezo vya kutathminia

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa wanavyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum, na mambo ambayo yanazingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40



Powered by: www.atikaschool.com

### 4.2.2 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)

Watahiniwa katika kitengo hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama **01-05** hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muwala na muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote, ama na misamiati jirani, au na mada husika. Udhaifu wao kimawasiliano huwakosesha kuikuza mada/ maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama **06-10** hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Hata hivyo, insha zao huwa na mategu mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujileza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka au kupungukiwa kimaudhui/upande wa mada na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili ( huwa na athari nyingi za lugha ya mama).

**Mtungo wa kwanza**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

Mualimu mku naibu wamwalimu mku walimu kinaja wa shulayatu naibu wakinaja na wanafunzi wao zangu Hamja mbo Naomba mnipe furosa hii ili niweze kuzungumzia mambo ma Chache

Leo nita waJulisha mambo machache ni upatikana anagalia hilishule Jambo lakwanza mkubwa wa shulayatu ana ni igiza niwa ambiya kuamba atatu lataa pipa nyingi za takataka Ili tosiwa

Tuki chafua shule nina waimiza kwama wakitulataa pipa za takataka tosiwa tokichafua shule yatu mathaka ya takataka Itatu patia ugonjwa wakolera

Amani imi zu pia niwa ambia tuki waka shole yatu ikiwa safi kushinda wangine atatulataa kila mtu zawadi maku Boa sana kisha atatuletaa mifarasi Ili ijae Shule yatu kisha takisha chaza atatu



Powered by: www.atikaschool.com

Wakea sabuni tumishughulikea tutanawa mikono yetu ili tusiweze kupatwa na ugonjwa kisha tukishawa kila mtu ata kula keky

Pamoja na maziwa ili tuweze kua wote wazuri ili ungejua kisi tudhika

Tambolatafu ata tu wakaa pahali pakuongea tukiisha jato alafu tuta anda kilasiku Kuchanganua tukishamaliza kuchanza tumefunga Alafu tukawa kena coho tola

Chao basi akasemalukika rambari yakuanza tutakiwa wakila mtu Baiskali na vitabu ili tuandale kusoma ku abidi watasoma tutawakiwa rangi kuanya barasa kila mtu atakuamu afionzuhi bali

Mlango za shule zitakuwa zikufungua na mdomo ukisa na nane tolota itaifungwa basi ikisazifungua utaingia ndani na itakua nyumbayaku ca teaa nacine nia glos i mukikula mutununua nyingine

Ili uwazaku tudisha tana tuki toka rambari ya kuanza tutanunua ina tatakilishi kilamtu ili uwe ku tumiani nyaka za kisha utarudisha siku ku tudishe vitabu

Basi na wa ambia tukika rambari ya kanza mari tutafanya mtihani na tarakilishi kisha wote miambimu tuki wa rambari mzuri tutabuhudika nakinyaji ca soda

Nawabiani tuta jangaua u wanja ukua mkubwa kisha iwana kifunika kama kia inanyesha tuna angu rotoni moda kisha inaji funga



Powered by: www.atikaschool.com

Hapondipa shule zingine zitakuja kuchazaa si katika vaja nyatu tutakuwa tukicaza tukiaza tena tutakua tukishindana na shule zingine ku ingia andai yamuli

Natuki tokamashindani watu wata kua wakikari bishua detasa zaitu zita wakua ikua kubaa na itakuaki babai wanu fuo zimia aja natana zita kindakima tatu tatu

yakuanzai itakua magari bi kusini na kaskazini kishatutakua tukishiranana

Mtahiniwa huyu ameielewa mada, msomaji anaweza kukisia kiini cha utungo. Hata hivyo, mada imeendelezwa kwa lugha hafifu mno. Ingawa ameandika kwa lugha ya Kiswahili, udhaifu wake wa kimawasiliano umemfanya kutoimidu mada hii. Ingawa kazi imepangwa ki-aya, mambo asemayo katika aya moja hayaelekei kuhusiana na ya aya ya awali. Uakifishaji wa kazi hii ni hafifu mno.Anachanganya herufi kubwa na ndogo hata katika neno moja.

Alama iliyotuzwa: **02**



Powered by: www.atikaschool.com

## Mtungo wa Pili

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.** KUDUMISHA USAFI SHULENI

"Hamjambo walimu na wanafunzi wenzango na thumaini mako na buher na afya mema. Mimi leo nikuhapa mbeleyeno kusungumza kuhusu usafi wa mazingira katiki shule hini.

Wanfunzi wenzango nataka kuwa ileza umuhimu wa usafi. Usafi unaeleza miaji kuhusu mtu hivyo basi tunafa kusafisha shule yetu.

Usafi unatukinga kutukana na mgunjawa mabaya. Wanfunzi wenzango mimi najuwa kuwamba si sote tunaelimishwa bbai ni dhari shahiri tuwena usafi katika shule yetu.

Mume funzuwa kuhusu usafi katika masomo nyenu kuwa ukusifu wa usafi una madhara menyi, basi hapa munapasuwa kudumisha usafi shuleni, munafa kuilewa walionena wahenga asiyesikia la mkuu hupujika mguu.

Wanfunzi ndio wanao takikana kudumisha usafi katika jamii, je? tutaweza aje kufanya hivi kama hata hatuwezi



Powered by: www.atikaschool.com

lahsh haye yote yamepita "Kitumuhimu ni kuwamba kutuka leo tutaporisha usafi katika shule huu.

Wanfunzi wenzanga nawaamba mujibi waji kusafisha popote tunaona uchafu katika Shule hii na tafadhali musitupe uchafu uwinuu popote iwe shuleni, barabarani na hata nyumbani hakuna mahali tunapaswa kutopa uchafu.

Elimu ni bahari, elimu ni mali na hata dui hawezi kuitatanisha, elimu ni hakimuwa akili. Kwa kuwa elimu ni mali, hapo basi tunafukuwana usafi kuwa sababu si ni wasomi na kuunyisha tunafukuwana usafi katika shuleni.

Nawashukuru kwa kunisikiliza kwa makini asanateni sana nawapege kila laheri."

Mtahiniwa huyu ameielewa mada. Ingawa insha hii ni bora kuliko ya awali, mtindo wake wa kujieleza bado ni hafifu mno. Mvuto wa insha yake umetingwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, Mathalani:

a) **thumaini** badala ya **tumaini**
b) **maku** badala ya **mko**
c) **buher** badala ya **buheri**
d) **mbeleyenu** badala ya **mbele yenu**
e) **kutukana** badala ya **kutokana**
f) **ukusifu** badala ya **ukosefu**

Uakifishaji wake mbaya mno unaishia kuvuruga muwala wa utungo wake.

Alama iliyotuzwa: **06**



Powered by: www.atikaschool.com

**Kundi la Pili (alama 11 – 20)**

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza/kusimulia kwa sentensi au kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa alama **11-15** huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo.Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/ lugha za mama.

Wanaotuzwa alama **16-20** huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi huutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.

**Mtungo wa Tatu**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

HOTUBA YA UDUMISHI WA USAFI

"Waziri wa Afya, Waziri wa Mazingira, Gavana, Seneta, Naibu wa chifu, Mwalimu mkuu, Naibu wa mwalimu mkuu, Walimu, wazazi, wafanyikazi wa Shule, Wanafunzi wenzangu Hamjambo? Nina Shukuru nyote kwa kuja hapa mapema. Sababu ya nyote kukusanyika katika huu ukumbi ni kwasababu ya jambo moja watu wengi hawazingatii ni kudumisha Usafi.

Watu wengi wameenda hospitalini mara nyingi na moja ya hizo sababu ni yakwamba labda mtu kwa nyumba yake vitu zimetapakaa kila mahali na ukienda chumbani mwake pa kulala manguo yake yametapaka au unaweza kupata lindi kubwa la manguo na



Powered by: www.atikaschool.com

mwishowe atapata magonjwa kutokana na hao wadudu wanao ishi mume humo mwa hilo ilindi la
mangua. Wengine wanopotaka msalani hawa oshi mikono na kesho asubuhi ndiye yule amekimbia hospitalini.

Tunataka serikali ipunguze unubuaji ya haya madawa ili watu watie akilini kwamba kupata dawa ya hizo tiba ni ngumu na pia bei ghali. Tukiendelea hivi mwishowe sote humu nchini tutajipata tunaishi tukitumia madawa kila saa na mwishowe watu wengi hasa watoto watafariki mapema kabla siku yao itimie.

Hapa majuzi nilitembelea shule moja ya bweni na wazazi wangu kwenda kusalimia rafiki wangu wa utotoni. Mazingira ya hiyo shule ilikuwa chafu madarasa yameja vumbi wanafunzi wote ni wakonda, kanbu kila mtu humo shule akona mikunjo mikunjo usoni na kama haumfahamu unaweza kumkosea kuwa yeye anafanana na mtu mzee aliye kula chumvi hadi akatosheka.

Wengine sare zao za shule zinafanana



Powered by: www.atikaschool.com

"Ihama za mtoto wa darasa la kwanza. "Mahali pao pakulala ni vigumu kwa mtu kitaona panya au kunguni baada ya labda dakika tano. Mwalimu mkuu ndiye huyo hajachana nywele zake. Kobi alilelivaa lina madoa labda ni ya supu au chai hatujui.

Kuna mashule mengini ambayo yana hakikisha kwamba usafi umedumishwa kwa hali ya juu. Nina wapa pongezi hayo mashule na waendele hivyo. Huo ndio mwisho wa hotuba yangu na ninatumaini mtadumisha usafi kwa hali ya juu. Asanteni kuwa kunisikiliza. Mwe na siku njema."

Mtahiniwa huyu anaonyesha kuielewa mada zaidi ya wale wa awali. Hata hivyo, utungo wake umejaa makosa ya sarufi na hijai ambayo yanaufanya kuwa hafifu. Makosa ya kisarufi yanayojitokeza ni kama vile:

a) **Hamjamboni**? badala ya **hamjambo?**
b) **Kwa nyumba** badala ya **nyumbani**
c) **Vitu zimetapakaa** badala ya **vitu vimetapakaa**
d) **Haumfahamu** badala ya **humfahamu**
e) **Manguo** badala ya **nguo**

Makosa ya kitahajia ni kama vile:

a) **Paa** badala ya **pa**
b) **Tapaka** badala ya **tapakaa**
c) **Wanao ishi** badala ya **wanaoishi**
d) **Kwa** badala ya **kuwa**
e) **Yakwamba** badala ya **ya kwamba**

Alama iliyotuzwa: **11**



Powered by: www.atikaschool.com

Mtungo wa Nne

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

UMUHIMU WA KUDUMISHA USAFI

Mwalimu mkuu, walimu, Viranja wenzangu na wanafunzi hamjambo? Asanteni nyote kwa kusanyika hapa leo. kwani nina uhakika kuwa mulikuwa na kazi ya kufanya mkijitayarisha kufanya mtihani wa mwisho wa mhula. Niliwaita hapa ili niongee juu ya usafi wa mazingira.

Viranja kutoka darasa mbalimbali walinijulisha juu ya jinsi mnavyo hifadhi mazingira yenu na kwa kweli ni jambo la kufanya mtu kupigwa na kibuhuti. Wewe kama mwanafunzi, unafikiria nini ukitupa taka kila mahali bila kujali? Haya mambo madogo madogo mnayofanya hutuambia mengi juu yenu. Mgeni akijaa hapa leo ataenda akiwa na fikira mbaya juu yetu.

katika mazingira tukona vitu kama mimea, mto, ziwa na wanyama. Yote hayo huathirika tusipodumisha usafi. Na badaye pia sisi tutakumbwa na shida. kwa jumla ugonjwa nyingi husababishwa na uchafu unaotokana na mazingira. Tukichafua mto na kutupa kila aina ya takataka ndani watu wengi huu taabika. Si mtu mmoja ndiye anayetumia maji hayo bali ni watu zaidi ya



Powered by: www.atikaschool.com

mia tano. Kwa mfano tunayo mto Fuzu, Ukiolopita karibu na shule yetu. Hutumiwa na watu ya kijiji hiki bila kusahau sisi wenyewe.

Hebu fikiria ni watu wangapi watakaoteseka kama mtu angejisaidia ndani ya maji. Samaki pia wataathirika na wengi watakufa. Kutupa karatasi kila mahali pia huweza kuleta shida kwa mmea unaokua. Kwa wanyama tunao wanaozurura mjini wakitafuta chakula kwenye biwi la taka. Wanyama hao kama vile mbwa huja huku shuleni kwa sababu ya uchafu huu wote. Wakiwapata shuleni wanafunzi wa darasa la tatu huenda kuwapa kibisha na kuweka maisha yao hatarini kwani wana weza kuwauma.

Tuwe wenye makini na watiifu na kujaribu kubadilisha jinsi tunavyo tunza mazingira. Ni hakika kuwa maneno haya hayajaanguka sikio la kufa kwa kuwa halisiki dawa. Muwe na siku njema.
Asanteni.

Mtahiniwa huyu amebainisha kuimarika zaidi.Anaitumia lugha kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wa awali. Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo wa kiwango wastani. Hata hivyo, hajaikuza mada ipasavyo. Kadhalika ana makosa mengi ya hijai na sarufi. Makosa ya hijai ni kama vile:

a) **kusanyika** badala ya **kukusanyika**
b) **huu taabika** badala ya **hutaabika**
c) **mnavyo hifadhi** badala ya **mnavyohifadhi**
d) **wana weza** badala ya **wanaweza**
e) **halisiki** badala ya **halisikii**

Alama iliyotuzwa: **20**



Powered by: www.atikaschool.com

**Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)**

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama **21-25** huwa na ubunifu wa kima cha wastani.Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo,, mtahiniwa huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama **26-30** huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu.Hata hivyo, insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.

**Mtungo wa Tano**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

Mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, walimu, wazazi ,wanagenzi wenzangu subalkheri. Nina bashasha belele kuwa mbele yenu leo hii kama kinara wa shule kuzungumza juu ya usafi. Natumai kuwa nyote mtafuata nitakayosema.

Kwanza, tunafaa tuzingatie usafi wa mazingira yetu. Tuvitupe vibaghalabaghala. Tunafaa tukumbuke kuwa mazingira hayo hayo tunayoacha ndiyo tutakayotegemea siku za usoni. Pia uchafuzi wa mazingira unaweza kueneza ugonjwa wa waba ambao huambukizana. Kwa hivyo, itakuwa ni gharama kutibu. Je, mnataka kupoteza hela kwa sababu tu ya mazingira chafu? Kumbuka jinsi wahenga walivyosema ki kobe walivyotakadamu, heri kinga kuliko tiba.

Pili, kama wanagenzi, twafaa tuyanadhifishe madarasa yetu. Kila wiki, tuyapige deki madarasa



Powered by: www.atikaschool.com

yetu ili kuzuia vumbi maara tyende tukauhikuwa na kifua kikuu. Tuhakikishe kuwa hatuzitupi karatasi ovyo darasani. Ikiwa hatutazingatia usafi darasani, tutaathiri wenyewe. Jambo hili litatendekaje? Hutakuwa makini darasani sababu ya vumbi na wadudu watakaohinikiza darasa. Hii itakuathiri kimasomo.

Tatu, tunafaa tuzingatie usafi wa miili yetu. Usipokuwa nadhifu, utakosa sahibu. Wote watakutoroka kwa sababu ya harufu utakayokuwa ukitoa. Utabaki pekee na kama sote tujuavyo jinsi machagina wa lugha walivyolonga, mkono mmoja haulei mwana waaidha jifya moja haliinjiki chungu. Tunafaa ikuzikata kucha maana kucha refu huficha viini ambavyo huweza kuusababisha madhara mwilini. Tupige meno mswaki, tuvipige viatu rangi ikiwa nywele zetu ziwe nadhifu.

Nne, tuzingatie usafi wa vyoo. Vyoo vichafu humilikiwa na nzi ambao husababisha madhara mengi kwa mwanadamu. Kwa hivyo kuepuka janga la ikipindupindu, ni lazima kama ibada tuzingatie usafi wa vyoo.

Usafi wa jikoni la shule pia unatakikana uzingatiwe. Iwapo mpishi atatumia vyombo vichafu, atawaletea wanagenzi wengi madhara makuu. Kwa hivyo, usafi wa jikoni lazima uzingatiwe. Pia, tusiviweke vyakula mfukoni. Mighairi ya hayo,



Powered by: www.atikaschool.com

turajaa kunawa kabla ya kula na baada ya kwenda msalani.

Mwisho, tuzingatia uwazi wa mwenendo wetu. Tukiwa wenye utovu wa nidhamu ambao ~~huenda taliba zinaruka je, basi hatutafanikiwa~~ maishani. Bighairi ya hayo, tutie bidii masomoni. Kumbuka kuwa elimu ndiyo nguzo ya baadaye.

Natumai kuwa nyote mtayazingatia yote niliyosema. Asanteni kwa kunipa fursa hii kuwahutubia, Rabli bin Rabira awatunikie baraka.

Mtahiniwa huyu amedhihirisha kuwa ameilewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo mpevu na kwa mvuto zaidi akilinganishwa na wa awali. Huyu pia ana makosa machache ya kimtindo akilinganishwa na wa awali. Anatumia lugha kwa wepesi zaidi. Hata hivyo, insha hii bado ina makosa ya sarufi na hijai.Kwa mfano:

a) **Tusitupe shaghalabaghala** badala ya **tusitupe taka shaghalabaghala**
b) **Huambukizana** badala ya **ni wa kuambukiza**

Aidha, uakifishaji usiofaa, na kuorodhesha hoja kwa kutumia maneno ya kuungia kama vile: kwanza, pili, kunaivuta nyuma kasi ya uwasilishaji na kuipoka insha mvuto.

Alama iliyotuzwa: **23**



Powered by: www.atikaschool.com

**Mtungo wa Sita**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

**Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

UMUHIMU WA USAFI

"Mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, mwalimu mwandamizi na wanafunzi wenzangu, masalkheri? Leo hii nimesimama kandamnasi yenu ili kuwahutubia kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni. Ningependa kumshukuru Rabana kwani amenipa afya ili nisimame hapa imara kama ngarange ya mvule.

Kwanza, usafi huwezesha mandhari kupendeza. Kila mja atabaki mdomo achama kama mja aliyeona mabaki ya Adamu na Hawa kwani kote kutakuwa kunapendeza ajabu.

Aghalabu wanafunzi wengi wamekosa kuhudhuria shule kwa kuwa ni wagonjwa. Kisa na maana wamepata taifodi, kolera, kipindupindu, kifuakikuu na bilhazia. Wamelazwa hospitalini karibu wiki moja.

Kwa mfano kipindupindu huambukizwa na nzi. Sisi huwacha chakula hapa na pale ovyo bila kukifunika. Nzi hawa hutua kwenye chakula chako. Hatimaye ukila chakula unaanza kuumwa na tumbo. Usilaumu yeyote kwani msiba wa



Powered by: www.atikaschool.com

kujitakia hauna kilio.

Wengine huambukizwa na kichocho wanapocheza ndani ya maji yaliyosimama. Wao hupelekwa hospitalini kwa kuwa wao si hayati si mamati. Wazazi wanatumia njenje sana kwa matibabu. Hata hivyo sisi hurudi kucheza pale pale. Tumekuwa sikio la kufa lisilosikia dawa wala kafara. Hata hivyo tutabaki tukisema laiti tungalijua.

Kila uchao hapa shuleni sisi hukagua wanafunzi. Kila mmoja lazima awe na kucha fupi, meno yaliyopigwa mswaki na nywele zilizochanwa. Si vizuri kuja shuleni na nywele zilizotimka timtim na za kipilipili.

Ni vizuri kupiga mswaki la sivyo mdomo wako utanuka fye mithili ya beberu aliyeanguka mtaroni. Darasani, daima dawamu usafishe dawati lako. Isitoshe, alasiri mfagie darasa lenu ili liwe safi. Kadhalika sare zenu za shule lazima ziwe nadhifu kama umande wa asubuhi na zinyooke twa!

Ni faradhi tudumishe usafi shuleni kwani tukiyatupilia mbali tutapata madhara chungu nzima. Kila



Powered by: www.atikaschool.com

mwanafunzi ni lazima awajibike kwani suala hii linatuathiri sote. Unapopata taka hapa na pale, moja kwa moja uliokate na kulitupa katika biwi.

Yeyote atakayefanya kinyume kwa kutupa taka ovyoovyo, ataona kilichomtoa kanga manyoya. Ninaona wakati umenipa kisogo kwa hivyo nitakomelea hapa. Ni matumaini yangu kuwa nyote mtafuata maagizo kama kwamba ni injili takatifu. Ahsanteni kwa kutega masikio yenu ndi! Mungu atawabariki kwa kuwanyunyuzia baraka teletele kama pishi la mchele."

Mtahiniwa huyu amebainisha ukomavu zaidi akilinganishwa na wa awali.Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo mzuri wenye mvuto kiasi. Amebainisha wepesi wa kuitumia lugha kufafanulia hoja zake. Hata hivyo insha hii bado ina makosa ya kihijai, kisarufi na msamiati. Kwa mfano, mtahiniwa anatohoa maneno ya Kiingereza hata pale neno hilo lina kisawe chake katika Kiswahili. Mifano ya msamiati wa aina hii ni:

a) **taifodi** badala ya **homa ya matumbo**
b) **kolera** badala ya **kipindupindu**
c) **bilhazia** badala ya **kichocho**

Aidha mtahiniwa huyu ana tafsiri ya moja kwa moja, kama vile **maji yaliyosimama** ambayo imetafsiriwa kutoka: *Stagnant water.*Baadhi ya misamiati imechopekwa tu, kwa mfano: **hupelekwa hospitali kwa kuwa wao si hayati si mamati.**

Alama iliyotuzwa: **26**



Powered by: www.atikaschool.com

**Kundi la Nne (Alama 31 – 40)**

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala au masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama **31-35** huitumia lugha kwa wepes zaidi. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama **36-40** huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu zaidi na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi au mitindo mbalimbali ya kujieleza ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi au mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.

**Mtungo wa Saba**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

HOTUBA KUHUSU UMUHIMU WA KUDUMISHA USAFI SHULENI.

**Wewe ni (kinara) wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

"Kinara msaidizi, viranja wa madarasa yote shuleni, wanafunzi wenzangu, hamjambo? Kwa kweli leo ni leo asemaye kesho ni mwongo. Kukusanyika kwetu hapa leo ni kwa nia na ari moja tu. Nimewaalika katika kikao hiki ili tuweze kuweka mikakati sambamba kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi hapa shuleni petu Tononoka.

Miongo ya miaka imeyoyoma na kuyeyuka kama barafu ilhali shule hii imezidi kudorora katika upande wa usafi. La! La! Nimechoka tiki! Kwa nini usafi wetu unazidi kuzikwa katika kaburi la sahau? Hakuna tena! Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha! Uchafu ambao umetawala katika shule hii sharti uzikwe katika lindi la sahau. Lisilo budi hubidi hali kadhalika hutendwa!



Powered by: www.atikaschool.com

Tafadhalini tazameni nje, jamani! Moyo wangu unajawa na huzuni kipindukia ninapoona shule yetu ikilingana na jaja au biwi la takataka. Wanafunzi wapendwa je, haya ndiyo mnayotaka yawe maisha yetu? Nimekataa abadan katan! Mazingira yetu yanaponadhifishwa, ebu jiulizeni, maisha yetu yatakuaje? Labda ninawazungumzia watu wasiojua la be wala la te. Hivi basi, wacha niwapashe nuru gizani kuhusu umuhimu wa usafi.

Kwanza kabisa, mazingira yetu yanapokuwa safi shule hupendeza kwa macho tu. Hata unapopiga milundi huku ukivuta hewa safi unahisi uzuri moyoni. Ebu niambieni, mngependa kukaa panapo nuka fe! Sidhani kuna yeyote ambaye angependa kuishi hapo. Hivi basi wanafunzi, tunaponadhifisha mazingira tunawavutia hata wavyele wa watoto wengine kuwaleta wana wao hapa ili kusoma.

Hali kadhalika, tunapodumisha usafi tunaweza kudunisha mawele ambayo yametuvamia kama jeshi la usubi. Tangu wiki iliyopita tumewaona wengi wakienda hospitalini maadamu wanaugua magonjwa ya kila aina. Hata wakati huu Juma (mwanafunzi mmoja) bado anaendelea kupata sijambo katika hospitali kuu ya Tbnonoka. Ole wetu! Chupa tunazozitupa kila mahali hujaa maji na kuwapa mbu nafasi ya kutaga



Powered by: www.atikaschool.com

mayai yao. Hali hii inawezesha malaria kusambaa kote.

Isitoshe, tunapodumisha usafi si kwenye mazingira pekee yake, bali hata kwenye miili yetu. Tangu jadi na jadadi tumefunzwa kuhusu usafi wa mwili. Mbona tumeyatia masikio komango? Mbona hatutaki kusikia la mwadhini wala la mteka maji msituni. Kumbukeni mwana msikivu haambiwi mchana kutwa. Kutoka leo sitaki kumwona mwanafunzi ambaye amechafuka. Lazima kila mmoja avae sare iliyosafi. Wengi wetu hurudia nguo moja kwa wiki tatu. Jamani, huyo ni aliye na akili timamu?

Nikirejea kwa utunzaji wa mazingira, tusisahau kuwa shule yetu ilitajwa ya kwanza katika mwaka wa alfeni na tatu kuwa shule safi zaidi nchini. Walionena walinena, mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Lazima kama ibada turejee huko. Tunataka watu wavutiwe na mazingira ya shule yetu. Hata wanaotaka kufunga pingu za maisha waje waazime uwanja wetu ili kufanya nikahi yao. Jamani wanafunzi wapendwa mwatakaje?

Walionena walinena, aliyekalia kigoda mtii. Basi nawasihi mfanye yote niliyowaambia na bila shaka shule yetu itaimarika na kuwa tajika. Lazima tuungane bega kwa bega kufanya usafi udumike huku shuleni. Msisahau



Powered by: www.atikaschool.com

kuwa inkono mmoja haulei mwana. vilevile kofi haziliii ila kwa viganja viwili. Asanteni."

Mtahiniwa huyu ameilewa mada na kuikuza kwa lugha komavu zaidi akilinganishwa na wa awali. Anajieleza kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wale wa vitengo vya chini. Ameteua msamiati mwafaka kulingana na mada yake.Mifano ya msamiati huu ni: *ari, kikao, mikakati, kudorora*.Hati yake ni nadhifu na inasomeka kwa urahisi.Hata hivyo, neno **sambamba** limetumiwa vibaya. Angetumia **ifaayo** au**mufti**
Insha hii ina makosa machache mno ya sarufi na hijai.Makosa ya hijai ni:

a) **kipindukia** badala ya **kupindukia**
b) **yatakuaje** badala ya **yatakuwaje?**

Aidha baadhi ya alama za uakifishaji kama vile kituo (,) zimetumiwa vibaya.

Alama iliyotuzwa: **34**

**Mtungo wa Nane**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

**Andika insha isiyopungua kurasa moja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

HOTUBA KUHUSU USAFI SHULENI.

**Wewe ni kiranja wa wanafunzi shuleni. Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi shuleni.**

"Mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, mwalimu mwandamizi, walimu wengine na wanafunzi wenzangu, sabalkheri? Leo hii, nina furaha kukithiri ya mwuki aliyekinaa kishazi cha samaki kupewa fursa na satua hii kusimama mbele yenu kidete. Wengi wenu bila shaka wana uchu ya kujua lengo langu. Nia yangu haswa ni kuzungumzia kwa mapana na marefu kuhusu usafi humu shuleni. Ni matumaini yangu kwamba mtayatega masikio ndi!

Usafi ni jambo muhimu sana katika maisha ya adinasi yeyote yule aishiye duniani humu. Hata hivyo, ni jambo la kuhuzunisha kwamba wengi wametupilia mbali usafi wa mazingira. Wanafunzi, msidanganywe katu kwamba usafi haufai. La! La hasha. Ninatumai hata Nuhu mwenyewe katika safina yake, licha ya kuwa na hayawani wale wote mle ndani, alijikaza kisabuni kuzingatia usafi. Je, ikiwa alimudu, sembuse wewe mwanafunzi?



Powered by: www.atikaschool.com

Nikiyatazama mandhari ya shule hii ya Tononoka, si Tononoka tena. Karatasi za vitabu zimetapakaa na kuzagaa kote kama cheche za moto katika jangwa. Isitoshe, maua yamenyauka. Ukielekea kwenye bweni za wasichana, sandarusi zenye taka zimetupwa ovyo. Jameni, kwani ushauri ule wote ambao walimu wetu wametupa ulikuwa kama kumwashia kipofu taa? Kwani si huko ni kuyaharibu mafuta tu?

Usafi wa mwili uzingatiwe kwanza kabla ya mazingira. Hakikisha kwamba kila asubuhi umejinadhifisha. Zaidi ya hayo, vitanda vitandikwe pindi tu unapoamka. Tafadhali, usimsubiri mwalimu wa zamu eti aje akukumbushe hususan wanafunzi wa darasa la nane. Soksi nazo zifuliwe baada ya kuzivua. Zifuliwe hadi zitakate.

Kuongezea hayo, karatasi zote zilizotapakaa ardhini ziokotwe na kutupwa kwenye mapipa ambayo yako katika kila kumba ya shule. Ni vyema ikiwa sandarusi zote vilevile zitapelekwa kwenye jaa ya takataka. Aidha, katika dahalia na bweni za maghulamu, tupapige deki, ikiwezekana kila Ijumaa baada ya masomo ya siku kukamilika. Kulaza damu ni kunyoosha mkono kuyakumbatia maradhi ambayo yanahusiana na uchafu. Kumbuka, tahadhari kabla ya hatari iwapo hutaki kuenda na ulelengoma.

Usafi usidumishwe katika mabweni tu bali pia madarasani. Madirisha yote yafunguliwe ili kuwe na hewa safi ; oksijeni. Hii husaidia vilevile wanafunzi kutosinzia darasani kwani endapo tu naumi inapoanza kumchukua, hupigwa na mzizimo wa upepo. Mbao zinazoandikiwa zifutwe baada ya somo moja



Powered by: www.atikaschool.com

kukamilika ili mwalimu mwengine akija asipoteze wakati kuufuta. Ama kweli, wakati ni mbango.

Pulikeni zaidi nyote. Ikiwa hukunisikiza tangu nilipoanza kuzungumza ninakuomba unisikize vyema. Hayati Bi. Wangari Maathai aliyafufua mazingira yetu kwa juhudi zake za nchiwa kujenga kichuguu za kupanda miti na kuzingatia usafi. Bila shaka, nyumbani pake usafi ndio uliotamalaki kote. Sababu yake kutokumbwa na magonjwa oyo oyo ni moja tu, usafi huu huu ambao tunazungumzia leo.

Wanafunzi wenzangu, ijapo shule yetu imedidimia katika usafi, nina imani kwamba tunaweza kuibadilisha hali hii. Waama, kuteleza si kuanguka. Tuanze kwa hatua hizi hafifu hafifu mwishowe tutafanikiwa. Chambilecho, mwanzo wa ngoma ni lele.

Kwa hayo yote ni matumaini yangu kuwa mwakani tutatangazwa kuwa shule bora katika usafi nchini. Asanteni kwa kunisikiliza. Mola awarehemee rehema kemkem."

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuikuza vyema na kwa ukomavu zaidi kimaudhui na kifani.Tofauti na watangulizi wake.Uteuzi wake wa mtindo unaipa insha yake shani ikilinganishwa na za awali. Anatumia vipengele vya kimtindo kama vile majazi, maswali ya balagha na ulinganishaji kwa ufanifu bila kuvuruga muwala na muumano wa mawazo yake. Tofauti na watangulizi wake, anahisika zaidi kuwa anawasiliana na hadhira yake moja kwa moja Mawazo yanatiririshwa kimantiki bila kukatizwa kwa uchopekaji mwingi wa msamiati ambao ulibainika katika insha za vitengo vya chini.Ametoa mfano wa mhusika aliyejitahidi kulinda mazingira na natija iliyopatikana kutokana na juhudi zake. Makosa machache yanayojitokeza ni ya uakifishaji.Pia, badala ya kutumia **kwani** katika, **Kwani si huko ni kuyaharibu mafuta tu?**, angetumia, **Je, huko si kuyaharibu mafuta?**

Kwa jumla hii ni insha ambayo ina uasilia na inaweza kuaminika kuwa ubunifu asilia wa mtahiniwa wa kiwango hiki.

Alama iliyotuzwa: **36**



Powered by: www.atikaschool.com

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano, msamiati wa magonjwa unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu magonjwa.Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri au kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali (ngazi/viwango) tofautitofauti za maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza au mitindo ya usimulizi..

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waonywe dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake.Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati au matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa.Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa, wasitumie kimoja tu.Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi. Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo, hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.



Powered by: www.atikaschool.com